## *Hutawahi kufanya lolote katika siku yoyote isiyoitwa leo.*

Mungu anataka kukubadilisha uwe katika mfano wa Mwanawe, Yesu. Inawezekana kwako kuanza maisha haya ya mabadiliko leo. Mtu mwenye hekima alisema kuwa safari ya maili elfu moja huanza kwa hatua ya kwanza. Iwapo u tayari kuchukua hatua ya kwanza na kuomba, Mungu yu tayari kuanza mpangilio wa mabadiliko leo. Endelea: kuwa mtu amwaminiye Mungu na kuitendesha imani yake kazi.

Hutawahi kufanya lolote katika siku yoyote isiyoitwa leo. Leo ni siku yako! Ifuatilie.

*Ombi la leo.*

Ewe Mungu, nifanye mtu anayekupendeza sana na uanze mabadiliko leo. Nipe neema ya kukumbatia majaribu ya maisha nikijua u nami hapa, ukiniongoza ninapoelekea pako pazuri kwa ajili yangu.

*Maandiko ya leo.*

Zaburi 95:7; Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, na kondoo za mkono wake.Ingekua heri leo msikie sauti yake.

Warumi 12:2; Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kami

## *Tunachofanya na tulicho nacho kinaonyesha sisi ni nani na tunaamini nini.*

Je, wewe watabirika? Mtu hujulikana kwa tunda la maisha yake. Hivyo basi ni haki tukihukumiwa kwa kile tulichotoa maishani kihistoria. Kwa nini mtu akutarajie kufanya tofauti na vile ulivyofanya awali? Haitoshi tu kungoja mambo yawe mazuri ili uanze kufanya mambo yaliyo sawa.

Unachofanya na ulicho nacho sasa kitaonyesha wewe ni nani na unachoamini. Kama hufurahishwi nacho, badilisha. Anza kuandika ukurasa mpya maishani mwako leo.

*Ombi la leo*

Baba, najua napanda mbegu leo ambazo zitakadiria mavuno yangu ya usoni. Nisaidie Bwana niwe na  subira, kuwa mkarimu na mwenye kuwawazia wengine,

na kuchukua nilicho nacho, kuanza nilipo na kufanya kadri ya uwezo wangu kwa ajili yako.

*Maandiko ya leo.*

Luka 16:10; Yeyote aliye mwaminifu katika mambo madogo, atakuwa mwaminifu katika mambo makubwa; na yeyote asiye mwaminifu katika mambo madogo, hatakuwa mwaminifu katika mambo makubwa

Waefeso 6:8;Kumbukeni kwamba kila mtu mwenye kutenda mema, awe mtumwa au mtu huru, atapokea tuzo lake kutoka kwa Bwana

## *Huku msamaha ukimgharimu msameheaji, urejesho ni jukumu la mkosaji.*

Kuna tofauti kubwa kati ya msamaha na urejesho. Msamaha ni haki. Urejesho ni jukumu. Kila mkosaji ana haki ya kiungu ya kusamehewa kosa lao na kila mwumini anaamrishwa na Mungu kusamehe kwa vile sisi, pia, tumesamehewa makosa yetu. Hata hivyo,msamaha haulingani na urejesho. Urejesho wa uhusiano uliovunjika huja baada ya upande uliokosa kukubali jukumu la kosa hilo na kufanya kila jaribio la ukweli na lenye maana kurudisha kilichopotea, kama inawezekana. Roho ya kweli ya toba na kuvunjika ni ishara kuwa mkosaji anaelewa thamani ya kusamehewa na anaahidi kuwa hatatenda kosa hilo tena siku zake za usoni. Iwapo umekosewa, samehe. Hata hivyo, ikiwa umekosa na ukasamehewa, kubali jukumu lako. Fanya hima kurudisha kilichopotea na kwa unyenyekevu ahidi kutorudia kosa lako. Labda Mungu atakupa urejesho wa uhusiano uliouharibu.

*Ombi la leo.*
Ewe Bwana, tafadhali nipe neema ya kuwasamehe wengine wanapokosa kutimiza matarajio yangu kwao au wanaponikosea. Pia, Baba, nipe neema na unyenyekevu wa kufanya niwezalo ili nirejeshwe kwa wale niliowakosea. Asante Awana, amina.

*Maandiko ya leo.*

Mathayo 6:14,15; Maana mkiwasamehe watu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia. Lakini msipowasamehe watu makosa yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.

Mithali 18:19; Ndugu aliyechukizwa ni mgumu kuliko mji wa nguvu. Na mashindano ni kama mapingo ya ngome

## *Wale tuliounganishwa nao wataashiria siku zetu za usoni.*

Mabinti wakwe wa Nuhu walikombolewa kutokana na kuangamia katika gharika na wakawa mama za ulimwengu mzuri mpya. Nini kiliwafanya kujulikana hivi? Si lingine ila uamuzi mkuu wa siku: nitaunganisha maisha yangu na nani? Kila siku watu huamua kuhusiana, shirikiana, chumbiana, kuoa, au pia kuwa marafiki wa karibu na wale wanaohusiana nao kwa uzuri au ubaya, kwa ufanisi au kuanguka.

Tuliounganishwa nao wataashiria siku zetu za usoni. Ni kweli pia tunawahusisha wengine tulio na uhusiano. Chuma hunoa chuma au pia yaweza kuifanya gutu. Unahusiana na nani? Chunguza uhusiano wako kupitia ukweli huu.

*Ombi la leo.*

Bwana Mungu, naomba uniongoze katika uchaguzi sawa kuhusu wale ninaotaka kuanza na kujenga uhusiano nao. Nifunze kuchagua marafiki wangu kwa hekima na unisaidie niwe rafiki na mhusika anayehitajiwa na wengine ili tufanye vyema kadri ya uwezo wetu kwa ajili yako. Niweke, Bwana, mbali na ushawishi mbaya.

*Maandiko ya leo.*

1 Wakorintho 15:33; Msidanganyike! Urafiki mbaya huharibu tabia njema

Mithali 4:14; usiingie katika njia ya waovu,wala usitembee katika njia ya wabaya.

## *Kuna mviringo wa maisha - mambo huanza na mambo haya huisha.*

Kila msimu wa maisha hutuletea fursa za kusonga mbele kutoka mambo ya awali yaliyokuwa mazuri, yaliyotuleta katika wakati huu, na kukumbatia mambo yatakayotuendeleza kutoka tulipo. Ili tujitayarishe vizuri kwa maisha na magumu yake yote yafaa tujifunze na tuwafunze wengine ukweli huu.

Kuna mviringo wa maisha - mambo huanza na mambo haya huisha. Hii ndiyo njia ya Mungu kwa maumbile yote. Kuna kitu kimoja kitakachosimama milele, Neno la Mungu.

*Ombi la leo.*

Nipe neema, Ewe Bwana, ya kubainisha misimu ya maisha yangu. Nisaidie kujua wakati wa kuacha jambo moja na kuanza lingine. Nipe amani katika mapito ya maisha na unipeleke katika siku yangu kuu.

*Maandiko ya leo.*

Mhubiri 3:1-2; Kwa kila jambo kuna majira yake,na wakati wa kila kusudi chinyi ya mbingu. Wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa, wakati wa kupanda, na wakati wa kun'goa yalio pandwa;

1 Petro 1:24-25; Kama Maandiko yasemavyo: "Kila binadamu ni kama nyasi, na utukufu wake wote ni kama maua ya porini. Nyasi hunyauka na maua huangukaLakini neno la Bwana hudumu milele." Neno hilo ni hiyo Habari Njema iliyohubiriwa kwenu.

## ***Kuna mviringo wa maisha - mambo huanza na mambo haya huisha. Kuna mzunguko wa maisha - katikati ya mwanzo na mwisho, kuna kupanda na kushuka.***

Barabara ya maisha imejaa mahali palipo nyororo na wakati mgumu, kona na mahali kulikonyooka, milima na nchi tambarare. Kama Yusufu, katikati ya kuzaliwa na kufa sisi pia tutapitia sehemu yetu ya wakati mzuri na wakati mgumu. Ni jukumu lako kuamua wakati upi utachukua kumakinika kwako. Mtazamo ni wa maana. Bilauri i nusu kujaa au nusu bila chochote? Hii ni shida yako au tunuku yako? Uamuzi ni wako.

Kuna mviringo wa maisha - mambo huanza na mambo haya huisha. Kuna mzunguko wa maisha - katikati ya mwanzo na mwisho, kuna kupanda na kushuka. Usivunjwe moyo, Mungu bado yu enzini mwake.

*Ombi la leo.*

Mungu, nisaidie nisizirai katika siku yangu ya majaribu. Nipe nguvu ya kujua pale kwenye kona, baada tu ya mlima, kukikucha, bado utakuwa enzini mwako na kila kitu kitatendeka kwa wema wangu.

*Maandiko ya leo.*

Zaburi 34:19; Mateso ya wenye haki mengi, lakini Bwana humponya nayo yote.

Zaburi 27:13; Naamini ya kuwa nitauona wema wa Bwana katika nchi ya walio hai

## ***Kuna mviringo wa maisha, kuna mzunguko wa maisha na kuna siri ya maisha - utavuna ulichokipanda!***

Sheria ya maisha kutoka Mwanzo 1 yasema kuwa kila kitu huzaa kinachofanana nacho, na mbegu ndani yao, na kuzaa matunda ya aina hiyo. Hakuna siri iliyo gizani au iliyofichwa kuhusu kuvuna mavuno. Kwa urahisi panda mbegu, kadri ya

kiasi unachotaka kuvuna, zimwagilie mbegu maji, palilia shamba hilo, kisha ungoje matunda kwa uvumilivu. Yatenda kazi si tu katika hali ya uhalisi, bali pia katika hali ya kiroho.

Siri ya maisha ni utavuna ulichokipanda. Je, wataka nini maishani? Ili wengine wawe wakarimu na watake urafiki nawe; wasaidie na mahitaji ya kimsingi; kutambua au kupandishwa cheo kutoka kwa wengine; kutia moyo; amani nyumbani mwako; furaha rohoni mwako; pesa kwa ajili ya siku zako za usoni? Panda!

*Ombi la leo.*

Bwana, nionyeshe mahali nilipopanda mbegu nisizotaka kuvuna na usababishe mavuno mabaya katika sehemu hizo … kisha Bwana, unipe wakati na hekima ya kupanda mbegu mpya katika shamba la maisha yangu. Nikumbushe, Bwana, kwamba kwa kila wazo, neno, na kitendo, ninapanda mbegu kwa ajili ya siku zangu za usoni na familia yangu.

*Maandiko ya leo.*

Mwanzo 8:22; Muda nchi idumupo, majira ya kupanda na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi, na wakati wa kusi, mchana na usiku, havitakoma

Waefeso 6:8; Kumbukeni kwamba kila mtu mwenye kutenda mema, awe mtumwa au mtu huru, atapokea tuzo lake kutoka kwa Bwana.

Wagalatia 6:7; Msidanganyike; Mungu hafanyiwi dhihaka. Alichopanda mtu ndicho atakachovuna.

## *Usichukue hali ya muda na kuunda shida ya kudumu.*

Karibu kila siku tunapata nafasi ya kufinyiliwa na majaribu madogo ya maisha. Sisi sote hukumbana na misukumo nyumbani, shuleni, kazini au na marafiki. Kutoshughulikia vikwazo hivi kutaruhusu misukumo kuwa zaidi ya shida zisizositirika.

Chukua ndoa kwa mfano. Watu wengi hutengana na kupeana talaka kwa sababu ya utofauti usioweza kurekebishwa ambazo zilianza kama kutokubaliana. Usiache maisha ya haraka au kukosa mwelekeo yakusukume uanze kuunda milima kutokana na miinuko midogo. Usiingie katika tabia ya kuchukua hali za muda na kuzifanya shida za kudumu. Badala yake, omba na urejeshe maisha katika mwelekeo sawa.
*Ombi la leo.*

Leo nahitaji msaada wako tena, Bwana. Nisaidie nisikwazwe na shida za kila siku na misukumo ya maisha. Nifunze jinsi ya kujielekeza na unikumbushe kuwa sio vitu vyote vinavyonihusu ni juu yangu. Nifanye mjenzi, si mharibifu, na unisaidie kuiona picha kubwa.

*Maandiko ya leo.*

Wagalatia 5:22-26; Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni mapendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifuupole na kuwa na kiasi. Hakuna Sheria inayoweza kupinga mambo hayo. Wale walio wa Kristo wameisulubisha hali yao ya kidunia pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zakeTukiishi kwa msaada wa Roho, na tuufuate mwongozo wake. Basi, tusijivune, tusichokozane wala kuoneana wivu.

## *Tafuta riziki, tengeneza maisha, leta utofauti.*

Watu wengine huchukua muda mwingi sana kutafuta riziki mpaka wanasahau kutengeneza maisha. Wana mishahara mingi na vyeo vya juu katika kampuni na jamii lakini watoto wao, wazazi na hata marafiki hawawajui. Wengine hutambua kuwa maisha ni zaidi ya kutafuta pesa na kununua vitu. Wao huweka raslimali ya wakati na kawi katika kujenga maisha kwa pesa wanazopata. Lakini maisha hayakomei hapo.

Mungu ametutengeneza kwa kusudi. Tunahimizwa na Neno na Roho kutafuta riziki na kutengeneza maisha ili tulete utofauti. Wewe wafanya nini kuleta utofauti wa kweli na wa kudumu?

*Ombi la leo.*

Bwana, nionyeshe kipaumbele maishani. Nifunze kuchukua kanuni za Neno lako na kutafuta riziki bora, kutengeneza maisha bora na kuleta utofauti mkubwa. Nisaidie kujua ninapopaswa kusema ndio na ninapopaswa kusema la. Niweke kando na kukimbia mbio zisizofaa na uniongoze kuelekea siku yangu kuu.

*Maandiko ya leo.*

2 Wathesalonike 3:10; Tulipokuwa pamoja nanyi tulikuwa tukiwaambieni, "Mtu asiyefanya kazi, asile."

1 Timotheo 5:8; Lakini kama mtu hawatunzi watu wa jamaa yake, hasa wale wa nyumbani kwake, basi, mtu huyo ameikana imani, na ni mbaya zaidi kuliko mtu asiyeamini.

Mathayo 6:20-21; Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba. Maana pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.

## *Kuna sababu kwa nini dirisha la mbele la gari ni kubwa kuliko kioo cha kando.*

Ninaambiwa ya kwamba mchezaji wa mpira wa magongo hujitokeza kugonga mpira na ya kwamba changamoto yake kuu sio yule anayerusha mpira lakini uwezo wake wa kumgonga. Anapogonga mzungo wa nyumbani mara ya mwisho, anasukumwa na matarajio ya kutaka kurudia tena. Kama alifaulu kugonga mara ya mwisho, kuna hofu ya kurudia. Changamoto kuu hufanyika katika mawazo ya yule mgongaji, na mrushaji pia. Vile tulivyofanya hapo awali, labda vibaya ama vizuri, inaweza kutuwekea viwango tunapotazama sana siku zilizopita na sipo kutazama kwa makini kwa siku zijazo.

Kuna sababu kwa nini dirisha la mbele la gari ni kubwa kuliko kioo cha kando. Hakika tunahitaji kuchungulia na mtazamo wa picha ndogo wa kule tumekuwa, lakini uwezo wetu mkuu bado uko mbele yetu. Wacha kukubali ya jana kutabiri ya kesho. Inua kichwa chako, fungua macho yako, na uangalie siku za usoni. Siku yako kuu ingali mbele yako!

*Ombi la leo.*

Nisaidie Baba nisichukue muda mwingi kutumaini au kuogopa niliyofanikiwa kufanya au niliyoshindwa kufanya awali. Siwezi kurudisha saa nyuma na kuishi tena au kubadilisha yangu ya jana. Nisamehe pale nilipokuangusha wewe, mimi na wengine. Nipe mtazamo na mpango katika siku zangu za usoni , kisha uniongoze katika yote niyafanyayo.

*Maandiko ya leo.*

Wafilipi 3:13; Ndugu, usijidhanie nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika ila natenda neno moja tu, nikiyasahau yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yalio mbele.

Wafilipi 4:13; Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.

## *Safari ni rafiki yako.*

Ni safari inayotuandaa kutenda katika uwezo wa mwelekeo wetu. Bila kuwa wakuu kiasi kila siku katika changamoto za maisha, huenda tusihitimu kupata fursa zisizokuwa za kiasi ambazo huja kwetu kila wakati. Safari ya maisha ya kila

siku pamoja na ming'ang'ano yake na ugumu wake ni mazoezi nafsi zetu zinazohitaji kuwa tayari kwa majaribio ya maisha.

Si Yusufu ama Daudi, wal Ruthu ama Esta, Petero ama Paulo wangeweza kujiandaa kutimiliza majukumu ya mwelekeo wao maishani kama haingekuwa kwa kuvutwa ama misukumo ya kuundwa ya safari zilizowaelekeza hapo. Safari si adui yako … ni rafiki. Acha kunung'unika, anza kukua.

*Ombi la leo.*

Mungu Mpedwa,s amahani kwa nyakati ambazo nimenung'unika ama kukasirika kuhusu safari yangu. Najua ya kwamba una mipango kwa maisha yangu na kwamba yote hutendeka kwa wema. Nisaidie nifahamu, nipatie neema ya kustahimili na uwezo wa safari yangu. Uwe mfinyanzi nami nitakuwa udongo.

*Maandiko ya leo.*

Yeremia 29:11; Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

Warumi 8:28; Tunajua kwamba, katika mambo yote, Mungu hufanya kazi na kuifanikisha pamoja na wote wampendao, yaani wale aliowaita kufuatana na kusudi lake.

## ***Kulaani giza hakutabadilisha lolote... washa taa.***

Haichukui karama yoyote kutambua na kunung'unika kuhusu kupungukiwa kwa kawaida kwa watu na mipango. Majaribu ni kuruhusu chukizoliwe msingi wa mazungumzo yetu. Hili zoezi ni la kukumbana na uhusiano ulio na afya na matunda na kusuluhisha shida.

Wana wa Israeli walikuza tabia mbaya ya kunung'unika na kulalamika kuhusu kila kitu ambacho hakikuwafaa ama kutokea walivyotaka. Punde tu, kila uamuzi wa viongozi wao ulipingwa na maendeleo yakasimamishwa. Kulaani giza hakubadilishi lolote, washa taa. Tunachohitaji kufanya na wazo letu zuri ni kupeana suluhisho. Ikiwa hatuna wazo zuri, tunapaswa kuwasaidia walio nalo.

*Ombi la leo*

Ewe Bwana, ninaweka imani yangu kwako. Nisaidie nisiwe mtu wa kulalamika. Nijaze na mawazo na suluhu ambazo zinaweza kufanya mambo yawe mazuri na kisha unipe kusikizwa na heshima ya wakubwa wangu, warika wangu ili niweze kuwapa mwongozo usiowatisha. Nifanye wa dhamana katika hali hii.

*Maandiko ya leo.*

Wafilipi 2:14; Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano.

Luka 21:15; kwa sababu mimi mwenyewe nitawapeni ufasaha wa maneno na hekima, hivyo kwamba zenu hawataweza kustahimili wala kupinga.

Zaburi 119:111; shuhuda zako nimezifanya uridhi wa milele, maana ndizo changamko la moyo wangu.

## *Wakati watu wanangoja mwondoko wa Mungu, Mungu anangoja mwondoko wa watu.*

Kupuuza jambo linalohitaji kuangaliwa halitafanya liondoke. Hata kugeuzia Mungu jambo analotarajia wewe ulifanye, halitaondoka. Kama hadithi ya wenye ukoma wanne katika 2 Wafalme 7; kukalia tu shida zako hazitasuluhishwa. Mungu anahitaji tuhusike na yeye katika shani za maisha. Bila kuingilia na kukumbana na adui zetu, huenda tusijue ushindi.

Wakati watu wanagojea mwondoko wa Mungu, Mungu anangojea mwondoko wa watu. Mungu anaweza na anataka kuchukua angalau kidogo cha juhudi zetu za kutoka ndani na kuzifanya zifaulu. Kama vile tunavuna tulichopanda, ni muhimu tuwe wa kutenda neno lakini sio wa kusikiza pekee.

*Ombi la leo*

Baba, nachagua kuwa mtenda wa neno la Mungu wala sio msikilizaji tu. Nisaidie niwe aina ya mtu anayeweza kutumainiwa katika matendo. Nipatie habari, uhuisho, na motisha ninayohitaji kuingilia na kuvamia. Nifanye mtendakazi pamoja na Roho wako Mtakatifu leo.

*Maandiko ya leo*

2 Wafalme 7:3c; Mbona tunakaa hapa  hata tufe?

Yakobo 1:25; Lakini mtu anayeangalia kwa makini sheria kamilifu ambayo huwapa watu uhuru, mtu anayeendelea kuizingatia, na si kuisikia tu na kuisahau baadaye, bali anaitekeleza, mtu huyo atabarikiwa katika kila kitu anachofanya.

## *Hakuna kufaulu kwa kudumu bila mrithi*

Kwa nini kile chote unachokijua kife na kiende kaburini na wewe? Maisha ni mbio za kupokezana vigongo; mchezo wa kikundi ambapo mmoja hawezi kushinda bila kikundi. Ni jukumu la kila mmoja kulea wanariadha wa mzunguko hou mwingine halafu kupokezana vijiti wakati bado wanaweza kukimbia.

Kwa kutilia mkazo sana kuweka kufaulu kwa mtu binafsi siku hizi, ndio maana tunaona chuki, wivu an tama zikiingilia jamii zetu. Chukua hatua nyuma na utafakari ni nini kutakuwa kufaulu kwako kwa kudumu. Tafuta mwanafunzi. Kuwa mlezi. Lea mwanariadha aliyehitimu kwa mbio zinazokuja. Pitisha kigongo. Hakuna kufaulu kwa kudumu bila mrithi.

*Ombi la leo*

Baba, nipatie mtu ambaye ninaweza ezeka. Nifunze niwe mlezi. Nipatie ujuzi wa kuendeleza yale ninayoyajua kuhusu maisha na umilele kwa wengine ambao siku moja watachukua nafasi yangu. Nisaidie kuweza kugusa maisha ya mtu kwa uzuri leo.

*Maandiko ya leo*

Mathayo 28:18; Yesu akaja karibu, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

2 Timotheo 2:2; Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

## *Mungu ana mpango; Atafaulu; Tuko na fursa ya kuhusika*

Kutoka shimoni hadi nyumba  ya Potifa, kutoka gerezani hadi hekaluni, Yusufu hakuwahi kuwa nje ya mpango wa Mungu kwa maisha yake. Daudi pia alienenenda katika njia ndefu iliyokuwa kombo ili afanyike kuwa mfalme wa Israeli kama vile Mungu alivyokuwa amenena. Wakati wa shida au ajali, inaweza kuonekena kana kwamba ni ngumu kuwazia kitu chochote kizuri kitokanacho na uchungu wetu.

Hata hivyo, sisi ni wa Kristo, ni lazima tuamini ya kwamba Mungu ana mpango, Atafaulu, na tushukuru kwamba tuko fna ursa ya kuhusika katika mpango wake. Hatuwezi kuruhusu ugumu wa kibinafsi kushinda mpango wa umilele wa Mwenyezi Mungu. Tunapokumbana na hali ngumu maishani, tunafaa tu kuamini na kutii.

*Ombi la leo*

Mungu, ninawezaje kuanza kuelewa hali za mpango wako kwangu, jamii yangu, na siku zangu za usoni. Mambo hayo naomba: Uwe mwenye rehema kwangu na kwa wapendwa wangu, kumbuka sisi ni udongo tu na na rahisi wa kuvunjika mikononi mwako. Tuepushe na maovu na ututumie kwa utukufu wako. Kama kawaida, sio mapenzi yangu ila Yako yatimie.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 45:8; Basi si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu; naye ameniweka kama baba kwa Farao na bwana katika nyumba yake, na mtawala katika nchi yote ya misri

Mathayo 26:39; Basi, akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akasali: "Baba yangu, kama inawezekana, aacha kikombe*fo* hiki cha mateso kinipite; lakini isiwe nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe."

## ***Changamoto zetu nyingi za maisha zaweza kukabiliwa kwa kukumbana na kweli na kwa kusema ukweli***

Kweli zaweza kuwa za kuogofya, za gharama, ama za kuvunja moyo na zinaweza hata kuelekeza lawama hadi kwako. Hata hivyo, ndiposa tupate tamati kamilifu, ni lazima tukumbane na kweli na tuseme ukweli … sio ukweli kulingana na mtazamo wako, ila kutokana na mtazamo wa Mungu.

Hakika maisha yanaweza kuwa magumu; tunaweza kupotoka; wengine waweza kufanya tushindwe; twaweza kushindwa wenyewe. LAkini Mungu ni mwaminifu, hata kama wengine sio waaminifu. Ana neno kwako. Neno kutoka kwa Biblia kuhusu hali yako ya sasa. Unaweza kumbana na kweli na kunena neno la Mungu maishani mwako.

*Ombi la leo*

Baba, najua unanipenda na hautawahi kutoa upendo wako kutoka kwangu. Nifunze neno lako. Nipatie imani ya kutulimaini zaidi ya vile ninavyotumaini maoni yangu, hofu zangu, ama vile wengine watakavyosema. Ninapokumbana na adui zangu kwa upanga wa Roho yako, nipatie ujasiri ninaohitaji kunena kwa imani.

*Maandiko ya leo*

Yohana 17:17; Waweke wakfu kwa ukweli; neno lako ni ukweli.

Waefeso 6:17; Upokeeni wokovu kama kofia yenu ya chuma, na neno la Mungu kama upanga mnaopewa na Roho Mtakatifu.

Waebrania 10:35; Basi, msipoteze uhodari wenu, maana utawapatieni tuzo kubwa.

## ***Inaweza kukugharimu sasa hivi kufanya jambo linalofaa, lakini inaweza kugharimu umilele kutokufanya***

Ushawahi waza ni nini inafanyikia nafsi nukta moja baada ya kuwa imechelewa umilele? Kuna sababu nyingi watu hupeana kwa nini wanakosa kufanya kilicho sawa. Baadhi ya hizi sababu nyingi zinagusia jaribio la kuepuka gharama ya haraka ambayo wakati mwingine inahusika kwa kufanya uamuzi uanaofaa.

Wako sawa! Inaweza kugharimu wewe kufanya jambo linalofaa. Kunaweza kuwa kuna gharama ya kulipa sasa hivi. Hata hivyo, kungojea kufanya jambo linalofaa huenda itakugharimu hata zaidi. Labda tulipe na siku zetu za usoni, ama sasa, ama tulipe sasa yetu na siku zetu za usoni. Uamuzi ni wako!

*Ombi la leo*

Ondoa hofu kutoka kwangu, Ewe Mungu, na unikomboe kutokana na roho wa kuahirisha. Nisaidie nifanye uamuzi unaoafaa, hata mbele ya gharama isiyodumu. Niwezeshe kuwa na nguvu katika msimamo wangu kinyume na kukubaliana na kuwa mwaminifu kwako bila hofu yamatokeo.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 4:15; Ila, sisi tukisema ukweli kwa moyo wa mapendo tutakua zidi katika kila jambo kulingana na Kristo ambaye ndiye kichwa;

Marko 8:35; Maana mtu anayetaka kuyaokoa maisha yake mwenyewe, atayapoteza, lakini mtu atakayepoteza maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Habari Njema, atayaokoa.

Kumbukumbu la Torati 30:19; nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako.

## *Pengine sababu hauwezi nunua unachotaka ni kwa sababu umeshanunua ulichotaka*

Shida moja na dola ni kwamba inatumika mara moja.tunaweza kosa kutambua ya kwamba tukisema ndio kwa ununuzi mmoja inaweza maanisha tunasema hapana kwa mwingine. Kununua ovyo ovyo ama kununua kwa msukumo si uwekezaji mzuri wa mitaji. Mungu anatutarajia tuwe wachungaji, sio wa kile tunachoona kama pesa zake, lakini pia hata wa kile tunachoita chetu.

Mara nyingi sababu hatuwezi kununua tunachotaka ni kwa sababu tayari tumeshajinunulia wenyeewe tulichotaka. Shida ni kuwa huenda hatutaki tulichonunua tena, ama angalau si sana tunavyotaka vile tunavyotaka sasa!

Mahali fulani inatubidi tupate mwelekeo wa matumizi. Una mwelekeo wa matumizi, ama yana mamlaka juu yako? Mungu anaweza kukusaidia!

*Ombi la leo*

Baba nikomboe kutokana na mitego ya maisha hasa katika eneo la fedha. Nionyeshe jinsi ya kupata mpango wa matumizi ambao utanifanya niwe mchungaji bora wa baraka unazopenda kunimwagia mimi. Jaza hazina zangu na utajiri wako na uniwezeshe niwe wa baraka kwa wengine.

*Maandiko ya leo*

Mithali 10:4; Atendaye mambo kwa mkono mlegevu huwa maskini; bali mkono wake aliye na bidii hutajirisha.

Mithali 10:22; Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo

Mithali 3:9-10; Mheshimu Bwana kwa mali yako, na malimbuko ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, na mashinikizo yako yatafurika kwa divai mpya.

## *Waweza kukosa kuona mabadiliko yakitendeka, lakini hata hivyo mambo yanabadilika*

Je, umeshawahi kuwa katika hali ya kurejelea pahali ambapo hujatembea yapata miaka kumi au zaidi? Pengine ushawahi kumwona rafiki wako wa jadi ambaye ilikuwa ni vigumu kumtambua. Mara nyingi mabadiliko ambayo yametukia kwa muda, ingawa ni nadra kutambulika katika mtazamaji makini siku kwa siku, yaweza kuoneakana kuwa ya kutatanisha kwa mtu ambaye hajakuwa akitazama kila siku. Ni kanuni ile ile tunayokumbana nayo katika hali yetu ya kiroho tunaposoma Neno letu la kila siku, kuungamana katika maombi kila siku, na kumtumikia Bwana kwa muda mrefu pasipo kukoma. Ingawa mabadiliko maishani mwetu na, pengine maisha ya marafiki wetu wa karibu na jamaa zetu yanaweza kutotambulika, hata hivyo, mabadiliko yanatendeka. Usikate tamaa wala kumruhusu adui akufanye ufikirie kwamba uunganisho wako wa kila siku na Mungu hauna matunda. Wewe, na wengine waliokuzingira mnabadilishwa mnapoendelea kutazamia Neno kamilifu la Mungu na utendeshe Neno hilo maishani mwako. Mabadiliko haya mara nyingi hutambuliwa na wale ambao bado hawajakuona kwa muda.

*Ombi la leo*

Baba, ninachagua kukutumainia katika maisha ya jamii yangu na marafiki na vilevile katika maisha yangu. Najua Neno lako na Roho linanitendea kazi kila siku

na ninabadilishwa niwe mfano wa Mwanao mpendwa. Asante kwa kunifanya zaidi kama wewe.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:1-2; Kwa hiyo, ndugu zangu, maadam Mungu ni mwenye huruma nyingi, nawasihi kwa moyo wote: jitoleeni nafsi zenu kwa Mungu kama tambiko iliyo hai, takatifu na yenye kupendeza. Hii ndiyo njia yenu halisi ya kumwabudu. Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

2 Wakorintho 3:18; Basi, sisi sote ambao nyuso zetu hazikufunikwa, twaonyesha kama katika kioo, utukufu wa Bwana; tunabadilishwa tufanane zaidi na huo mfano wake kwa utukufu mwingi zaidi. Hiyo ni kazi yake Roho wa Bwana.

## *Nguvu za dhambi zimo katika siri*

Mungu ni mwanga na ndani yake hakuna giza kamwe. Hakuna anayeweza kuenda na arejeshe mkebe wa giza. Giza, kwa urahisi ni ukosefu wa mwangaza. Hii ni kanuni ilei le ya kuwepo kwa dhambi. Dhambi, kwa urahisi ni ukosefu wa haki. Dhambi hutendeka tunapo ondoka katika haki ya Mungu. Dhambi hupoteza nguvu zake tunapokiri hiyo dhambi kwa Mungu, tutubu, na turudilie usawa na Mungu.

Dhambi hujificha kwa urahisi mahali ambapo hapana mwangaza. Nguvu za dhambi zimo katika siri. Usikubali dahmbi ikuweke katika utumwa. Dhambi hupoteza nguvu unapoileta kwa Mungu na umulike mwangaza wa neno maishani mwako.

*Ombi la leo*

Ewe Baba wa Mbinguni, ninajua nimekosa na ninakiri sasa dhambi zangu kwako. Ninaziwacha na kugeuka mbali nazo. Nisamehe, Eeh Bwana, na unioshe kutokana na ukosefu wangu wa haki. Nioshe kwa maji ya Neno lako Takatifu. Dhambi haitanishikilia tena. Asante Bwana.

*Maandiko ya leo*

Yohana 3:20; Kila mtu atendaye maovu anauchukia mwanga, wala haji kwenye mwanga, maana hapendi matendo yake maovu yamulikwe.

Warumi 6:14; Maana, dhambi haitawatawala ninyi tena, kwani hamko chini ya Sheria, bali chini ya neema.

1 Yohana 1:9-10; Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi Mungu ni mwaminifu na mwadilifu, naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote. Tukisema kwamba hatujatenda dhambi, tutakuwa tumemfanya Mungu mwongo, na neno lake halimo ndani yetu.

## *Jambo la muhimu na la faida tumeshawahi kukutana nalo huenda ikawa kwa mara ya kwanza ni jambo baya na mzigo usiostahili*

Siku moja mtu alichukua vijana wake wawili mjini. Wakatazama baba yao akifanya biashara na vile alivyoingiana na wachuuzi. Baba yao akapata mankuli ya mchana na akakaa akaongea na vijana wake kuhusu somo la siku hiyo. Alikuwa anawaandaa siku moja kuchukua nafasi katika jamii.

Walipokuwa wakipita mitaani, walikutana na mtu aliyekuwa amehukumiwa akielekezwa kwa adhabu yake. Mhukumiwa huyo akaangushwa na uzito wa mzigo wake. Wale wana wakatazama baba yao akitishwa na askari na kulazimishwa kubeba msalaba wa yule mhukumiwa. Kama Simoni wa Kurene, kitu cha muhimu na chenye faida tunachokumbana nacho chaweza kuonekana kama mzigo usio wa haki na mbovu. Inaaminika ya kwamba wana wa Simoni baadaye walifanyika viongozi wa kanisa la hapo awali.

*Ombi la leo*

Bwana, nisaidie kutolalamika ninapoamurishwa kubeba mzigo wa mtu mwingine. Nipe nguvu na huruma ninazohitaji katika huduma Yako kuu isiyoshindwa kwako, na watoto wako.

*Maandiko ya leo*

Mathayo 27:32; Walipokuwa wakienda, wakamkuta mtu mmoja jina lake Simoni, mwenyeji wa Kurene, wakamlazimisha kuuchukua msalaba wake Yesu

Wagalatia 6:2; Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza sheria ya Kristo.

## *Mungu atakupa wewe kipimo sambamba kwa kile anaweza kukupa kupitia wewe*

Ushawahi hisi kana kwamba vijito vya maisha yako vimesimamishwa? Kama utembezi wa uwepo wa Mungu na baraka zimezuiliwa? Iwe ni fedha, ufunuo, hekima, ama furaha, Mungu hazuilii kitu chochote kizuri kutokana na wanaotembea imara mbele zake. Pengine unafaa kujichunguza.

Jambo moja kati ya zile kanuni za kweli za Neno la Mungu ni kwamba Mungu atakupa wewe kipimo sambamba kwa kile anaweza kukupa kupitia wewe. Unapojichunguza, hakikisha unatazama kuona kama umekomesha utembezi wa wema wa Mungu maishani mwako kwa kukataza kile kinachotiririka kwako kitiririke kupitia kwako. Wakati mwingi tunaweza kuwachilia maji ya utulivu katika bahari ya maisha yetu kwa kuhakikisha mikondo yake ni misafi inatiririka huru. Unatamania nini zaidi? Fanya kutwalia wengine naye Mungu atahakikisha amekutwalia.

*Ombi la leo*

Ninataka kuwa baraka Bwana. Nitatoa muda wangu, talanta, na fedha vile utakavyoniongoza. Fungua madirisha ya mbinguni na unimwagilie baraka zako. Nijulishe amani Yako na uwepo Wako. Nifunze Neno Lako lililo hai.

*Maandiko ya leo*

Luka 6:38; Wapeni wengine wanavyohitaji, nanyi mtapewa. Naam, mtapokea mikononi mwenu kipimo kilichojaa, kikashindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika. Kwa maana kipimo kilekile mnachotumia kwa wengine ndicho ambacho Mungu atatumia kwenu."

Mithali 19:17; Amhurumia maskini humkopesha Bwana; naye atamlipa kwa tendo lake jema.

Waefeso 6:8; Kumbukeni kwamba kila mtu mwenye kutenda mema, awe mtumwa au mtu huru, atapokea tuzo lake kutoka kwa Bwana.

## *Tazamia jibu lako linalofaa kwa Mungu*

Mungu anatarajia mengi kutoka kwetu. Lakini, Alitupa Mwana wake, Neno lake, na Roho wake kutufunza, kutuongoza, na kutulinda. Hatuna visababu vya kutufanya kutotii amri zake. Hakuna hali ya maisha inayompa mtu haki ya kutotilia maanani Neno la Mungu. Hatuwezi ruhusu matendo ya wengine kutuamulia jinsi ile tutatenda kiungu.

Tukikumbana na majaribu, mitihani, majaribio, na misukumo ya maisha, lazima tunoe mitazamo yetu kwa jawabu zuri kwa Mungu. Kwa kujiuliza wenyewe Yesu angelifanya nini, ni mwelekeo mzuri kwa shida yoyote.

*Ombi la leo*

Baba, nataka kukufurahisha zaidi ya mimi mwenyewe ama wngine. Nisaidie Bwana kuona kupitia hali zilizochanganyikiwa kwa kanuni za neno lako. Katika

kila hali ya maisha nifunze kutazama jawabu langu linalofaa kwako bila kuangalia wengine wanafanya nini.

*Maandiko ya leo*

Warumi 14:10-12; Kwa nini, basi wewe wamhukumu ndugu yako? Nawe, kwa nini wamdharau ndugu yako? Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Maana Maandiko yanasema: "Kama niishivyo, asema Bwana kila mtu atanipigia magoti, na kila mmoja atakiri kwamba mimi ni Mungu." Kwa hiyo, kila mmoja wetu atatoa hoja yake mbele ya Mungu.

## *Maisha yetu yote yanaonesha kile tunachoamini*

Kile tunachofanya na kile tulicho nacho kinaamua sisi ni kina nani na yale tunayaamini. Mtu hajali kile unachojua mpaka ajue unajali. Usidnganyike, mtu hawezi kufia kitu asichoishia.

Maisha yetu yote yanaonyesha kile tunaachoamini. Unaandika hadithi ya wajukuu wako wataisema siku moja. Kwa kila uamuzi unaouongeza katika kurasa ya hadithi hiyo inaweka kumbukumbu ya maisha yako. Fanya uamuzi wa busara.

*Ombi la leo*

Mungu, ulisema mtu mwenye hekima atawacha milki kwa watoto wa watoto wake na kwamba jina zuri ni bora kusikika kuliko dhahabu na fedha. Baba, nataka hadithi ya maisha yangu ieleze kuhusu mtu ambaye alibarikiwa na Wewe na akawa baraka kwa wengine. Nionyeshe kufanya maisha yangu yajukumike.

*Maandiko ya leo*

Mithali 22:1; heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi; na neema kuliko fedha na dhahabu.

Mithali 13:22; mtu mwema huwaachia wana wa wanawe urithi; na mali ya mkosaji huwa akiba kwa mwenye haki

1 Yohana 3:7; Basi, watoto wangu, msikubali kupotoshwa na mtu yeyote. Mtu atendaye matendo maadilifu ni mwadilifu kama vile Kristo alivyo mwadilifu kabisa.

## *Mungu anataka tuhusike kwa miujiza yetu*

Kutoka kwa dirisha na kikombe cha mafuta kidogo na unga kidogo mkononi katika 2 Wafalme 4, mpaka kwa Naamani mweye ukoma katika 2 Wafalme 5,

Mungu anatutarajia tumtumainie Yeye na tutende kwa Neno Lake. Lazima tuanze pale tulipo, tuchukue tulichonacho, na tufanye ya muhimu tuliyonayo. Mungu atakumbana nasi na asfanye  utofauti.

Mungu anataka tuhusike kwa miujiza yetu. Lazima tuwe watendaji waaminifu wa kazi Mungu na sio wasikilizaji tu wa neno. Mungu atabariki kazi ya mikono yako ili kila kitu unachofanya kitanawiri.

Ombi la leo

Ewe Mungu, bariki kazi ya mikono yangu. Naweka nadhiri kwako kwamba sitakuwa mzembe, ama wa huahirisha, lakini nitaanza pale nilipo, nichukue nilichonacho, na nitafanya ya muhimu nayo. Nipatie miujiza ninapoendelea. Niogeze mimi ni baraka zako nyingi. Nitakuwa mtendaji wa neno lako.

Zaburi 127:1; Bwana usipoijenga nyumba waijengao wwafanya kazi bure. Bwana usipolinda mji, yeye aulindaye akesha  bure.

1 Wakorintho 15:58; Basi, ndugu zangu wapenzi, simameni imara na thabiti. Endeleeni daima kuwa na bidii katika kazi ya Bwana, mkijua kwamba kazi mnayofanya katika utumishi wa Bwana haitapotea bure.

Zaburi 1:3; na tuvipasue vifungo vyao na kuzitupia mbali nasi kamba zao.

### ***Yesu atakuwa Bwana, kwa kushinda ama kwa kuidhinishwa***

Hakuna nguvu katika ulimwengu zilizo kuu zaidi kuliko nguvu za Mungu ambazo amempa Mwana wake, Yesu. Siku moja, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri ya kwamba Yesu ni Bwana. Huu ni ukweli na utatendeka.

Yesu atakuwa Bwana kwa kushinda ama kwa kuidhinishwa. Wale ambao wanamjua na kumpenda wapeane maisha yao kwa Bwana bila tisho wala hofu. Hata hivyo, wale wanaoshikilia usumbufu wao na mapenzi maovu, hukumu inawangoja ambapo nafsi ya waliopotea zitalia pamoja na kila kiumbe, Yesu ni Bwana! Mpe haki yake leo … Atashinda hata hivyo.

*Ombi la leo*

Baba, nimemkubali Mwana wako kama Mwokozi wangu na sasa ninataka kuyakabithi upya maisha yangu Kwake. Yeye ni Bwana wangu. Kwa furaha ninampa nadhiri yangu kumtumikia Yeye, kumpenda na kumtii kama Bwana wangu na Mfalme ajaye hivi karibuni.

*Maandiko ya leo*

Luka 6:46; "Mbona mwaniita `Bwana, Bwana,` na huku hamtimizi yale ninayosema?

Mathayo 7:21; "Si kila aniambiaye, `Bwana, Bwana,` ataingia katika Ufalme wa mbinguni; ila ni yule tu anayetimiza mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.

Wafilipi 2:10-11; Ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.

### *Kuanguka chini sio kushindwa – kukaa chini ndio kushindwa*

Fikiria, tunatembea pamoja, tukielekea kanisani. Pengine nijikwae kwa kitu njiani na nianguke. Hata kama sikuumia sana, kiburi changu kimeadhirika na nimeabika. Ujaribu kunisaida, lakini niendelee kulala pale nilipoanguka, hatimaye nikushawishi uendelee na safari bila mimi.

Wiki ijayo, tukielekea kanisani tena, unikute nimelala pale pale nilipoanguka. Nikiwa mdhaifu na mchafu kutokana na yale niliyopitia, nikuhesabie janga la kushindwa kwangu. “ Nilijaribu, nikafanya bidii, lakini singetembea kuelekea kanisani.” Je ushauri wako utakuwa nini? Inuka! Kuanguka chini sio kushindwa lakini kukaa chini ndio kushindwa.

*Ombi la leo*

Mungu nifunze kujiona mwenyewe kupitia macho yako. Mimi ni mtoto wako, najifunza kutembea na kukimbia katika mbio za maisha haya. Nisaidie niepuke kushindwa, haswa wakati nimeanguka na ninahitaji kuinuka tena, nijikung’ute mwenyewe na nijaribu tena. Asante Bwana.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 37:23; hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, naye aipenda njia yake.

Mithali 24:16; kwa maana mwenye haki huanguka mara saba akaondoka tena; bali wasio haki hukwazwa na mabaya

### *Wasioamini jehanamu huenda wasiwe wa kudhuru kuliko wale wanaoamini na hawana himizo kuwakataza wengine*

Ni Mungu wa aina gani itamgharimu kumtuma Mwanawe wa pekee afe msalabani kukuokoa wewe kutokana na kitu ambach hakiko? Rafiki yangu, kuna jehanamu! Kutengwa kwa milele kutokana na Mungu katika ziwz la moto, sambamba na kifo na malaika wote walioanguka, itakuwa ndio hali ya umilele ya kila mwandamu atakayekataa kumtambua Yesu kama Bwana wakati wana fursa.

Ni jukumu la kila muumini kuwa mshuhuda, sio mambo ya kushtusha ya jehanamu, lakini wa baraka za mbinguni na jinsi ya kufika huko. Wasioamini jehanamu huenda wasiwe wa kudhuru kuliko wale wanaoamini na hawana himizo kuwakataza wengine. Sisi ambao tunashikilia mwangaza lazima tuuangaze katika njia za umilele wa maisha kwa wengine. Je, unafanya sehemu yako?

*Ombi la leo*

Baba, nafsi zimeketi leo kwenye hatari. Watenda kazi wanahitajika. Andaa mioyo kwa mavuno na unitume kwenye mashamba. Nionyeshe mtu nimshuhudie leo. Fungua mlango na unipe maneno sawa ya kusema. Sitaiabikia injili ya Yesu Kristo.

*Maandiko ya leo*

Ufunuo wa Yohana 20:15; Mtu yeyote ambaye jina lake halikupatikana limeandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika ziwa la moto.

Luka 10:2; Akawaambia, "Mavuno ni mengi, lakini wavunaji ni wachache. Kwa hivyo, mwombeni mwenye shamba atume wavunaji shambani mwake.

Warumi 1:16; Sioni aibu kutangaza Habari Njema; yenyewe ni nguvu ya Mungu inayowaokoa wote wanaoamini: Wayahudi kwanza, na wasio Wayahudi pia.

### ***Hazina ya baraka za Mungu maishani mwako inapatika katika shamba la mapenzi ya Mungu katika maisha yako***

Mungu ana mapenzi na makusudi katika maisha yako, shamba lililo na rotuba kwako wewe kukuwa. Kuna mahali pa baraka na kutwalliwa kwa kila mtu na yale yote anayopitia. Abrahamu alimwita Mungu, “Yehova Yire.” Zaidi tu ya ufahamu ya kwamba, “Bwana atanitwalia”, ndio maana ya kweli ya hili jina. “Katika mlima wa Bwana atanitwalia.”

Mungu amekwisha tutwalia kwetu mahali pale anapotaka tuwe katika kila majira ya maisha. Hazina ya baraka za Mungu maishani mwako inapatika katika shamba la mapenzi ya Mungu katika maisha yako. Kumbuka, hata hivyo, ni vigumu kupata dawa ya kutibu hali ya kijiografia katika maumbile. Mabadiliko unayohitaji huenda yakamaanisha kubadilisha kwa hisia zako ama shukurani zako.

*Ombi la leo*

Mungu, nataka kuwa katikati ya mapenzi yako kwa maisha yangu. Ninenee na unionyesho pale unataka niwe, vile unataka niwe, na kile unachotaka nifanye. Nipe ndoto na maono, ninenee kupitia Neno lako na Roho wako. Dhibitisha mapenzi yako kwangu.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 22:14; Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-Yire, kama watu wasemevayo hata leo, katika mlima wa Bwana itapatikana.

1 Wafalme 17:9; Ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemuagiza mwanamke mjane wa huko akulishe.

Zaburi 84:11; Kwa kuwa Bwana, Mungu, ni jua na ngao, Bwana atatoa neema na utukufu. Hatawanyima kitu chema hao waendao kwa ukamilifu.

### ***Sio kuvutia kwetu kunakofanya tuwe wa dhamana kwa Mungu, bali ni tabia yetu***

Hali hii ya kuvutia imelinganishwa na watu ambao wana njia ya kushinda kuwahusu. Tabasamu, ujasiri, na kwamba wanajua wanakokwenda na wanfahamu jinsi ya kufika hapo. Hizi ndizo sababu watu wahaisi vizuri kuwa karibu nao. Watu hawa wa kuvutia, hujivutia kusanyiko.

Hata hivyo, sio kuvutia kwetu kunakofanya tuwe wa dhamana kwa Mungu, bali ni tabia yetu. Wakati kuvutia kunaweza kutusaidia kufika kiwango fulani cha ufanisi, kutambulika, ama kukubalika, itagharimu tabia kukaa hapo. Zaidi ya tabia za kuonekana nje zinazopendeka, kujitolea kwa ndani kwa kweli, uwazi, uaminifu, na tabia za kikristo zitasaidia kukuza tabia zetu. Tabia ni vile Mungu anavyotuona.

*Ombi la leo*

Ombi langu la leo, Baba, ni ya kwmba nikufurahishe kwa maneno yote ninayosema na kufanya. Naweka nadhiri kwako kuwa mtu aliye na tabia kama za Kristo. Sitaruhusu msukumo wa maisha kuniamulia wajibu wangu. Nisaidie nisijikwae na kuanguka. Fanya moyo wangu nyumba yako.

*Maandiko ya leo*

Mathayo 23:26-28; mfarisayo kipofu! Kisafishe kikombe ndani kwanza, na nje kitakuwa kisafi. Ole weny, walimu wa sheria na Mafarisayo, wanafiki! Mko kama makaburi yaliyopakwa chokaa ambayo kwa nje yanaonkana kuwa mazuri, lakini ndani yamejaa mifupa ya maiti na kila namna ya uchafu. Halikadhalika, ninyi mnaonekana na watu kwa nje kuwa wema, lakini kwa ndani mmejaa unafiki na uovu.

### ***Wakati mwingine jambo la kiungu mtu anaweza kufanya ni kulala***

Katika Biblia nzima, Mungu anahimiza, hata kuamuru, ya kwamba watoto wake watambue umuhimu wa nyakati za kupumzika na mapumziko. Hakuna kitu kinaweza fanya upya mawazo na mwili kama kupumzika kutokana na shughuli za kila siku za maisha.

Hakuna katika historia ya mwanadamu watu wamekuwa na shughuli nyingi, wakikimbia toka kitu kimoja hadi kingine, wakiamini ya kwamba siku moja mambo yatapunguza kasi. Kuongezeka kwa hizi mbio ni misukumo ya kazi, shule, jamii, madeni, na maisha ya kawaida. Huenda ikawa ugonjwa wa akili na mwili ndio maana uko juu kila wakati. Wakati mwingine jambo la Kiungu mtu anaweza kufanya ni kulala. Chukua mapumziko! Ni njia ya Mungu.

*Ombi la leo*

Baba, nisamehe kwa kutokuruhusu hekima yako katika eneo la mapumziko kibinafsi. Nisaidie kuepukana na shughuli na nitenge wakati wa muhimu wa kufurahia safari, na nifanywe upya kwa mkondo mwingine. Chukua kusumbuka kwangu kwote na ujaze maisha yangu na amani.

*Maandiko ya leo*

Mathayo 11:28; Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.

Luka 10:39-42; Martha alikuwa na dada yake aitwaye Maria; huyu aliketi karibu na Yesu akisikiliza mafundisho yake. Lakini Martha alikuwa anashughulika na mambo mengi. Basi, akamwendea Yesu, akamwambia, "Bwana, hivi hujali kwamba dada yangu ameniacha nishughulike peke yangu? Mwambie basi, anisaidie." Lakini Bwana akamjibu, "Martha, Martha, unahangaika na kusumbuka kwa mambo mengi. Kitu kimoja tu ni muhimu. Maria amechagua kitu bora zaidi ambacho hakuna mtu atakayemnyag`anya."

Zaburi 127:2; kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, na kukawia kwenda kulala, na kula chakula cha taabu; Yeye humpa mpenzi wake usingizi.